JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA**

*Unapojibu tafadhali taja:*

***Kumb.Na.*** MDC/I/20/21/VOL.II/12 13 Novemba, 2023

# TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi moja ifuatayo:-

**MTENDAJI WA KIJIJI III: NAFASI 01**

**SIFA ZA MWOMBAJI:**
Kuajiriwa wenye cheti cha kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIJI III:**

- **i.** Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- **ii.** Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamzi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- **iii.** Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- **v.** Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- **vi.** Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- **vii.** Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- **viii.** Kusimamia, kukusanya na kihifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- **ix.** Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- **x.** Kupokea, Kusikiliza na Kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- **xi.** Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
- **xii.** Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**MSHAHARA:**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji III kina mshahara wa TGS B kwa mwezi.

**MASHARTI YA JUMLA:**

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji ambaye ni mtumishi wa Umma apitishe maombi yake kwa mwajiri wake.
- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- "Testmonials", "Provisional Results" "Statements of results" nk. Hazitakubalika.
- Waombaji waweke picha moja katika barua zao za maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NECTA.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 27/11/2023 saa 9:30 Alasili.
- Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapo chini:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga,
S.L.P. 194,
**57483, Kigonsera, RUVUMA**

<u>**NB:**</u> Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo ni:- **www.mbingadc.go.tz**

Juma Haji Juma
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**MBINGA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MBINGA

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika
Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi
S.L.P. 2320,
**DODOMA.**

" **Tovuti ya Halmashauri <u>www.mbingadc.go.tz</u>**

" **Mbao za Matangazo**